

**Huyu ni Mwanangu mpendwa
ninayependezwa naye...**



**MSIKIENI
YEYE!**

*"Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea." (Mathayo 18:11) **Msikieni Yeye!** Si estás perdido...necesitas salvarte ...de la ira de Dios. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." (Matendo 4:12)*

*"Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu." (Warumi 10:3) **Msikieni Yeye!** Unahitaji haki ya Mungu - Bila hiyo utaenda kuzimu sasa hivi. Pokea haki yake Mungu. "Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu." (I Yohana 1:9) Sasa hivi, tafadhali umwombe Yesu Kristo aje moyoni mwako, akuokoe na akusamehe makosa yako. "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka." (Warumi 10:9)*

*"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe." (Mathayo 24:35) **Msikieni Yeye!** Maneno yalionenwa na Yesu hudumu ya kweli leo, kesho, na hata milele. "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu." (Waebrania 9:27) Je, umefahamu ya kwamba mstari huu wa Biblia umedhihirishwa kuwa kweli. Ni ukweli mtupu ya kuwa siku moja utakufa...na ni kweli utahukumiwa na maneno yalionenwa na Yesu!*

atika Biblia kuna amri iliyotoka kwa Mungu..."**Msikieni Yeye!**" Mungu alinena hayo kuhusu mwanawe Yesu. Kama hujui yatakayotokea kwako baada ya kufa. Basi soma kikaratasi hiki.

"Na mtu akiyasikia maneno yangu, asiyashike, mimi simhukumu; maana sikuja ili niuhukumu ulimwengu ila niuokoe ulimwengu. Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amuhukumuye; neno hilo niliolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho." (Yohana 12:47-48) **Msikieni Yeye!** Ukimkataa Yesu, utahukumiwa na neno lake siku moja.

"Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakufa katika dhambi zenu, kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." (Yohana 8:24) *"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."* (Warumi 3:23) **Msikieni Yeye!** Usipomwamini Yesu utakufa na dhambi zako.

"Mimi ndimi njia na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi." (Yohana 14:6) **Msikieni Yeye!** Yesu alisema huwezi kufika mbinguni ila ya yeyhakuna njia nyingine.

"Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu." (Yohana 3:18) **Msikieni Yeye!** Kama hujaamini Bwana Yesu, weweumeshahukumiwa tayari katika ziwa la moto.

UMEKATA KAULI GANI?

Ni chaguo langu kumkataa Yesu. *"Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni."* (Mathayo 10:33) **Msikieni Yeye!** *"Asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."* (Yohana 3:36b)

Nimekubali kumkiri Yesu awe Mwokozi wangu. *"Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu."* (Yohana 10:28) *"Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."* (I Yohana 5:12) **Msikieni Yeye!**

Tafadhali tuma karatasi hii kwetu utujulishe ya kwamba baada ya kuisoma, umekata kauli ya kumpokea Yesu awe Mwokozi wako.

Jina _____

Anwani _____

Mji _____ Umri _____



FELLOWSHIP TRACT LEAGUE

P.O. BOX 164 • LEBANON, OH 45036

www.fellowshiptractleague.org © Tract 8110 (Swahili)

All tracts free as the Lord provides. Not to be sold.